

**TAWALA ZA MIKOIA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANSPAA YA TABORA**

SHULE YA SEKONDARI NDEVELWA

S.L.P 1067

TABORA

14 /12 /2020

KUMB Na . NSS /S2940 /TMC /03

JINA LA MWANAFUNZI:.....

KATA YA NDEVELWA

MANISPAA YA TABORA

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NDEVELWA
KIDATO CHA KWANZA 2021**

1.0 UTANGULIZI

Nimefurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2021 katika shule ya Sekondari Ndevelwa. Shule ipo katika kata ya Ndevelwa umbali wa kilometa 01 kutoka makao makuu ya kata eneo la Chang'ombe.

Muhula wa kwanza masomo yanaanza tarehe 11 /1 /2021 na unatakiwa kuripoti siku hiyo mwisho wa kuripoti ni tarehe 18 /1/2021.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SALE ZA SHULE

A. WAVULANA

- i. Suruali rangi ya damu yam zee iwe pana miguuni (isiwe model) na mifuko ya wima (rangi ya kitambaa nimeambatanisha).
- ii. Shati nyeupe (Tetroni) ya mikono mifupi isibane mwili
- iii. Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunika miguu vyenye visigino na sori fupi, visivyo chongoka kwa ajili ya darasani, viwe na kamba za kufunga
- iv. Soksi nyeusi
- v. Tai ndefu inayo fanana na kitambaa cha suruali
- vi. Sweta rangi ya damu ya mzee

B. WASICHANA

- i. Sketi rangi ya damu yam zee (rangi ya kitambaa nimeambatanisha) iwe na marinda makubwa ya kulala yaliyo elekea upande mmoja na mkanda usiozidi inchi 2,urefu wa sketi ipite magoti na isibane mwili.
- ii. Shani nyeupe tetroni ya mikono mifupi isibane mwili wake kuonesha nguo za ndani
- iii. Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunika miguu, vyenye visigino na sori fupi visivyo chongoka kwa ajili ya darasani (viwe na kamba ya kufunga)
- iv. Tai ndefu inayo fanana na kitambaa cha sketi
- v. Sweta rangi ya damu yam zee
- vi. Soksi nyeupe ndefu isiwe na mchanganyiko wa rangi
- vii. Rangi ya hijabu ifanane na sare ya shule kwa wale wanaopenda kuvaa hijabu

2.2 . Daftari kubwa 11 (counter Books , Quire 2) karamu za wino, penseli na mkebe wa Hesabu.

3.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa na sheria Na. 10 ya mwaka 1995 Aidha , inazingatia miongozo yote inayo tolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia. Yenye dhamana ya elimu Nchini naofisi ya Waziri mkuu TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

- a) Heshima kwa viongozi , wazazi , wafanyakazi wote wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima .
- b) Mahudhulio mazuri katika kila shughuli ndani nan je ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
- c) Kushiriki kwa makin kufanya maandalio ya jioni (Preparations)
- d) Kuwahi katika shuhguli za shule na nyingine utakazopewa
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani nan je ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
- f) Kutunza usafi wa mwili ,mavazi na mazingira ya shule
- g) Kuvaa sale ya shule wakati wote unapo takiwa
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- i) Kutunza mali za umma

3.1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababishwa kufukuzwa au kusimamishwa shule :-

- a) Wizi
- b) Uasherati na ushoga
- c) Ubakaji
- d) Urevi na matumizi na madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi , cocaine ,mirungi kubeli N.k
- e) Kupigana au kupiga
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- g) Kudharau Bendera ya Taifa
- h) Kuwa mjamzito au kupata mimba
- i) Kuoia au kuolewa
- j) Kutoa mimba
- k) Kugoma ,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuluga Amani na usalama wa shule au watu
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi
- m) Kuwa na simu ya mkononi , kuja na simu shuleni

3.2. Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi

- a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na mganga Mkuu wa Hospital ya serikali . fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakapo ripoti shuleni.
- b) Fomu ya mzazi kukili kukubaliana na sheria , kanuni na maelezo mengine yatakayo yolewa na shule.

4.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo /maagizo haya na kuyatekeleza kwa uaminifu.

Hongera sana nakutakia maandalizi mema !

Karibu sana

.....

Siwema w. Jonas

Mkuu wa shule

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

Ndevelwa Secondary School

P.O. Box 1067

TABORA

Date :

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

Must be completed Government Medical Officer

Student's full name

Present Age

Blood Test.....

Stool Examination

T.B Test

Asthma.....

Eye Disorder.....

Nose Disorder.....

Ear Disorder.....

Skin Disease.....

Anemia.....

Chest

Operations

Serious accidents Disease.....

Pregnancy.....

ADDITIONAL INFORMATION e.g. physical defects or impairment, chronic or family

Disease.....

I certify that I have personally examined Mr. / Miss.....

And found him / her fit /unfit to pursue studies

Signature.....

Designation

Officer rubber stamp.....